# Gazeti la Kimataifa

## Waabuduo Damu ya Kristo

...Kwa Neno Lako...

Lima, Peru 5–28 Luglio 2017

Mwaka XXI – N. 10, Novemba 2019

ASC Mawasiliano ya Kimataifa – Uongozi Mkuu - Via Maria De Mattias, 10 - 00183 Roma

www.adoratrici-asc.org redazioneasc@adoratrici-asc.org

# Sinodi ya Amazon: wito wa kweli kuelekea upyaisho

Mhariri

Katika mwezi huu uliowekwa wakfu kwa Bikira Maria, Mama wa Yesu, kuna harakati nyingi katika Kanisa zinazoshuhudia uwepo wa Roho akituongoza katika mchakato wa kubadili ulimwengu.

Tukio muhimu zaidi linaloendelea sasa ni Sinodi ya Amazon.

Ni wakati maalum wa neema kwa sababu ni wakati wa kuwasikiliza maskini, kusikiliza kilio cha damu kinachosikika kutoka kwa viumbe wenyewe. "Viumbe vyote vinaugua, navyo vina utungu pamoja hata sasa," Mtakatifu Paulo anatukumbusha. (Rm. 8:22)

Ni kilio kinachopanda kutoka kwa wenyeji ambao wapo hatarini kupoteza utambulisho wao bila matarajio yoyote ya siku za usoni kwa sababu ya uharibifu wa msitu wa Amazon, mapafu yenye umuhimu mkubwa kwa maisha ya sayari yetu.

Kazi hiyo inahusu Amazon, lakini mada zinazojadiliwa, zinazoanza na utangazaji wa Injili hadi uangalifu kwa walio wadogo, kutoka kwenye mipaka mipya ya huduma hadi kwenye heshima ya Uumbaji zinahusu Kanisa la ulimwengu na familia nzima ya wanadamu.

Tunamshukuru sana Papa Francis kwa kuitisha Sinodi hii kwa sababu wanadamu wote unahusika na Amazon. Katika ulimwengu wetu wa utandawazi, sote tumewekewa jukumu moja la kumhudumia kila mmoja, kushirikisha mambo muhimu katika ustawi wetu wa kutembea pamoja kwa sababu uhai wa mmoja ni uhai wa kila mtu.

Kuweka mpangilio mzuri wa vitu pia inamaanisha kuwa ni hali ya kusikiliza kishindo kutoka katika ulimwengu wote pamoja na uchungu wake wote, upweke, udhaifu, kwa kuwa ushuhuda wa tumaini unaotokana na utangazaji wa nguvu iliyoletwa na damu ya Yesu .

Kwa hivyo, Kristo anatualika kuamsha tena hamu ya kujiruhusu kubadilishwa ili tusikwame kwenye yale yanayoonekana, kwa kile kinachojaza macho yetu na siyo mioyo yetu. tunaombwa twende zaidi ya kukata tamaa, kutokuwa na hakika, uhakika, kifo chenyewe.

Katika safari hii Maria, Mwanamke mwenye kusikiliza, anatufundisha kuendelea kukesha pamoja na Yesu na katika Yesu na, kwa Neno la Mwana, anatualika tuwe na macho yaleyale, matazamo uleule, na hisia zilezile ili tuweze kuishi maisha mapya na yaliyobadilika ndani Yake.

***Sr. Maria Grazia Boccamazzo, ASC***

## Muhstasari

*Mhariri*

◇ Sinodi ya Amazon: wito wa kweli kuelekea upyaisho 1

*Nafasi kwa Uongozi Mkuu*

◇ Miaka Hamsini ya Historia Tanzania 2

*Toka Ulimwengu ASC*

◇ Sinodi ya Amazon 3

◇ Mwaliko wa Kushangaza 3

◇ Matoleo ya Viazi Vitamu 4

◇ Kutangazwa Mtakatifu Kardinali Newman huko Roma 5

◇ ASCs "kurudi" Morino 6

◇ Miti ya Mizeituni ya maarifa 7

◇ "Taa tano za Mungu" 8

*Nafasi kwa JPIC/VIVAT*

◇ Sauti za Amazon zilisikika huko Roma 9

*Ndani ya Shirika*

◇ Kalenda ya Uongozi Mkuu 10

◇ Siku za kuzaliwa: Tusherehekee Maisha 10

◇ Mikutano ya Region 10

◇ Waliorudi Nyumbani kwa Baba 10

# Miaka Hamsini ya Historia Tanzania

Wakati ambapo tumeweza kushirikishana matukio mengine kupitia vyombo vya habari, Uongozi Mkuu ulishiriki katika maadhimisho ya miaka 50 ya uwepo wa ASC nchini Tanzania pamoja na Sr. Dani Brought na Sr. Maria Grazia Boccamazzo.

Septemba 21 ilichaguliwa rasmi kwa ajili ya adhimisho la Misa iliyotanguliwa na sala ya siku tatu. ulikuwa wakati wa neema ambao ulituwezesha kutafakari juu ya uaminifu wa Mungu kwa historia na kwa kila Mwabuduo, siyo tu Masista watanzania. Kama Askofu Mkuu Beatus Kinyaiya, O.F.M.Cap, wa Jimbo Kuu la Dodoma, alivyosema wakati wa mahubiri yake, jubilei ni tukio la kumshukuru Mungu kwa zawadi na uaminifu wake, lakini pia ni fursa za kutathmini na kuamua kusonga mbele kwa kujitoa upya. Ushiriki wa watu wengi, marafiki, wafanya kazi, wanawake na watoto, wale wanaofaidika na huduma ya Waabuduo hawakuonyesha shukrani yao tu kwa Masista bali pia upendo wao kwa Maria De Mattias na upendo kwa Karama ya Waabuduo. Mh. Angelina Mabula, Naibu waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na Mkuu wa Mkoa wa Chemba Mh. Simon Odunga, walishukuru na kusisitiza umuhimu wa uwepo wa Waabuduo katika eneo wanalohudumia. Kujitoa kwao kwa ajili ya heshima ya mtu kumechangia maendeleo na ustawi wa nchi nzima, na wanaendelea kufanya hivyo.

Mnamo Novemba 22, 1969 Masista Romana Sacchetti, Delfina Gnerre, Nicolina Scattaglia, na Angelina Palmigiani, Waabuduo wanne wa mishonari walipanda meli, wakasafiri kutoka bandari ya Brindisi. Baada ya safari ya mwezi mzima kupitia bahari, walifika katika bandari ya Mombasa (Kenya). Hapa Wamishonari wa Damu Azizi, ambao walikuwa wamefika Tanzania kwa mwaliko wa Askofu Anthony Jeremiah Pesce, C.P., walifika katika bandari ya Mombasa kwa lori kuwakaribisha Masista. Kuanzia wakati huo na kuendelea huko Manyoni, shukrani pia kwa ushirikiano wa Wamishonari, Masista walianza kazi yao ya uinjilishaji vijijini, na kwenye parokia kwa kujibu kilio cha Damu ambacho kiliwaita kuwatumikia maskini, Tanzania. Kuanzia Manyoni hadi Chibumagwa, kutoka Itigi hadi Dodoma, kutoka Morogoro hadi Dar Es Salaam, hadi Vikawe, hadi Mafuiane (Msumbiji) hadi Cesena (Italia) Waabuduo wanaendelea kupeleka upendo wa Kristo kupitia utume wao wa elimu, msaada kwa waathirika wa Ukimwi katika Kijiji cha Matumaini, na huduma ya kiroho, kibinadamu na afya. Wanaendelea wakaribishaji wapendwa kwa ishara ya tumaini kila mahali na kwa kila mtu, hasa kwa masikini.

Sr. Josephina Paul pia alisherehekea miaka yake ya 25 ya nadhiri za kitawa kwenye tukio hili kwa roho ya shukrani, shamrashamra na furaha.

Uwepo wa Sr. Marisa Nardoni, mmishonari Tanzania kwa miaka zaidi ya ishirini, ulimpa kila mtu nafasi dhahiri ya kupata mang'amuzi ya muunganiko kati ya wakati uliopita na wa sasa. Hii ilikuwa sababu ya furaha na kuguswa kihisia kwa wengi.

Uwepo wa Sr. Marisa Nardoni, "jiwe la pembeni" la Region, hakika ulichangia katika kusherehekea tukio hilo. Aliwajibika katika malezi ya makundi ya kwanza ya Waabuduo na alikuwa mtunzaji wa chipukizi la miaka ishirini na tano ya historia.

Leo kuna Waabuduo watanzania 72 walio na nadhiri za daima na 15 wenye nadhiri za muda wanaoishi katika Jumuiya 12, zikiwemo moja nchini Italia (huko Cesena) na moja nchini Msumbiji (Mafuiane). Kuna miito mingi pia.

Masista kwa sasa wanajishughulisha katika nyanja ya elimu kwenye shule za msingi na sekondari, kwenye katekesi parokiani na katika huduma ya wagonjwa kwenye zahanati na hospitali hasa kwa umakini pekee kwa watoto yatima waathirika wa ukimwi kwa njia ya mpango wa tiba na matibabu ya kuzuia maambukizi ya ukimwi kwa akina mama na familia leo, katika Kijiji cha Matumaini huko Dodoma.

Katika kupanda meli hiyo, Masista labda hawakufikiria kile tunachoweza kutafakari leo, Shukrani kwa Mungu: kwa kuwa zawadi isiyopimika kwa jirani yetu mpendwa na mti wenye kuzaa matunda popote unapopandwa.

***Sr Maria Grazia Boccamazzo, ASC***



Eneo la Bara: Amerika
Region ya Manaus

## Sinodi ya Amazon

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mungu kwa wazo la Papa Francis la kuitisha Sinodi ya Amazon, na kukutanisha mamia kadhaa ya Maaskofu ambao hutoa huduma yao katika Amazon.

Sinodi imeufanya Ulimwengu wote uwe makini kwa sababu ya shida kubwa za Amazon: Kisiasa, kiuchumi, kijamii, kidini, kiikolojia na pia kwa sababu ya moto ambao unaharibu msitu wake.

Katika Jumuiya zetu za ASC, Sinodi imekuwa ikifuatiliwa vizuri, haswa kupitia vyombo vya habari vya Kikatoliki, vya Umma, na Mikutano iliyoandaliwa na vyama vya Mashirika ya kidini na ya waandishi wa habari wa Parokia mbali mbali. Askofu wetu Erwin Krautler CPPS amekuwa mstari wa mbele kwa sababu Papa alimwita Roma miezi kadhaa iliyopita, haswa kwa kujifunza juu ya hali ya watu wa kiasili waliotengwa ambao wanahitaji umakini mkubwa.

Mada nyingine ambayo ilifanyiwa kazi sana kwenye Sinodi na Padre Erwin na Kardinari P. Claudio Hummes OFM, ilikuwa ni ombi la Upadre kwa wanaume waliofunga ndoa (VIRI PROBATI) kwa ajili ya kutoa huduma huko Amazon.

Ombi hili limesisitizwa kwa sababu Mapadre ni wachache na watu wanahitaji huduma ya Ekaristi.

Baada ya kuwasikiliza Maaskofu hawa, Papa alisema "ulizaneni kwa mkazo na mlifanye wazo hili likomae kwenye Sinodi na muwasisitize watu waendelee kusali."

Namalizia kwa kiitikio cha Wimbo ambao tumeuimba. "Kila kitu kinategemea uhusiano wa kila mmoja wetu kwamba tu wamoja. Yote yameunganishwa katika nyumba yetu ya pamoja ambayo ni Ulimwengu.

***Sr. Marília dos Santos Menezes, ASC***

## Mwaliko wa kushangaza

Siku moja ya kupendeza Sista Mônica Borsa Lima, ASC wa Region ya Brazil, alipokea mwaliko wa kushiriki chakula cha jioni kilichoandaliwa na wanafunzi wake wa zamani wa mji wa Nova Olinda Do Norte.

Waabuduo walikuwa wamehudumu huko Nova Olinda kwa miaka kadhaa na Sr. Mônica, ambaye alikuwa muuguzi, alifanya angalau kila kitu, pamoja na kuwa mkunga wakati wa kuzaliwa watoto wote waliozaliwa wakati wa miaka hiyo. Pia alihudimia kama daktari wa upasuaji wakati ilipobidi kwa sababu wakati huo hakukuwa na hospitali kama ilivyo leo. Lakini, Bwana Mwema alikuwa pamoja naye.

Sr. Mônica alikubali mwaliko huo kwa furaha kwa sababu ilikuwa ni zaidi ya miaka arobaini tangu amwone mmoja wa "watoto" wake.

Yeye na Sr. Vitoria Zanes walifika kwa ajili ya chakula cha jioni kilichoandaliwa katika Hoteli nzuri ya Amazonas. Kulikuwa na watu hamsini na zaidi ambao walianza kumkumbatia na kujitambulisha na kumwonesha familia zao: watoto, waume au wake. Ilikuwa ni zamu ya kukumbatia iliyochukua zaidi ya saa na nusu kwa sababu kila mtu alitaka kuonesha shukrani zake.

Kikundi hicho kilimpa kadi nzuri yenye jina la "BLESSED ENCOUNTER"

"Mpanzi alitoka kwenda kupanda mbegu ..." Mt. 13: 3

Ndani yake iliandikwa:

**kamwe hatujachelewa sana kukuambia ASANTE, kwa sababu umekuwa ndani ya mioyo yetu daima na ndani ya mioyo ya wanachama Watendaji Wamishonari wa Waabuduo Damu ya Kristo.**

**Watoto wako milele**

Makanali wawili wa jeshi la Brazil walikuwa kati ya wale waliokuwepo, kulikuwa na mwanamke wa miaka 95 na wengine wenye umri zaidi ya miaka 60. Kanali Vitor Alencar alimshukuru kwa niaba ya wote.

Ilikuwa pia fursa kwa watu wengi kukutana na marafiki zao tena, na zaidi kumwona Sr. Mônica

Chakula cha jioni kilichojaa furaha kilikuwa saa 2:00 p.m. na kuhitimishwa kwa kusali sala ya Baba yetu na Salamu Maria kwa kushikana mikono kila mmoja.

Sr. Mônica alishirikisha kwamba watu wengi walitoa machozi ya shukrani kwa Bwana kwa zawadi ya maisha na urafiki.

Tunamshukuru Bwana kwa mema yote ambayo Masista wetu walifanya na wanayoendelea kufanya kwa ajili ya watu wahitaji zaidi.

***Sr. Clara de Albuquerque, ASC***

# Matoleo ya Viazi Vitamu

Parokia yangu, Mt. Vincent De Paul huko St. Louis, ilianza mkesha Jumatano jioni kwenye ngazi ya kanisa letu kusali kwa ajili ya watu na hali kwenye Mpaka. Nusu saa ya tafakari fupi ilifuatiwa na muda wa kutoa maombi na nafasi ya kuwaita watu kwenye mpaka ndani ya mioyo yetu.

Wiki iliyopita, walipokusanyika wanaparokia, mmoja wa wakazi wetu wa barabarani, akiwa na nguo chafu iliyochanikachanika, alilikuja na kupita kwenye milango ya kanisa, akiwa amebeba chombo cha chakula cha plastiki.

Mmoja wa wanaparokia na mimi tulimfuata ndani kanisani ili kuona kama alikuwa anahitaji chochote. Kimyakimya akaweka chombo juu ya meza ya matoleo iliyoko nyuma ya kanisa, alikataa kuongea na sisi, na akaondoka. Greg na mimi tulifungua chombo hicho na kugundua kuwa kilikuwa na viazi vitamu vilivyopikwa. Kwa jinsi nilivyoona hakikuwa kitu cha kawaida, nilitaka sana kumpata mtu huyo kuona kama angependa nguo tofauti kutoka kwenye nguo zetu zilizoko chumba cha chini. Akiwa na mavazi yake yaliyochanika alikuwa wakitembea kwa kasi kuelekea kwenye eneo la maegesho, tulipotoka nje kumwendea, tulimkosa.

Tulipokaa kimya kwenye ngazi za kanisa kwa ajili ya sala ya pamoja, tulisikia mingurumo ya magari yaliyotembea kwa kasi, umbali kidogo toka kwenye jengo, nilitafakari matoleo ya viazi vitamu.

Meza hiyo ndogo ya marumaru, ambayo kwa kawaida hutumika kuweka mkate na divai, sasa lilikuwa na chombo cha viazi vitamu, zawadi yake ya pekee kwa kanisa. Kama mfano wa sadaka ya mjane maskini kwenye Injili, labda yeye pia alitoa yote aliyokuwa nayo, hata kama ni viazi vitamu badala ya pesa au mkate au divai.

Mungu, mimi, sipokei na kuhukumu thamani, mastahili, na umuhimu wa zawadi hiyo. Sawa na watu waliokusanyika kwenye ngazi katika hali ya ukimya walisali kwa ajili ya ndugu zetu huko Mpakani, mkazi huyu wa mitaa yetu ya jiji kimyakimya aliacha viazi vyake vitamu, sala yake ya jioni.

Tutarudi wiki baada ya wiki kusali kwa ajili ya Mpaka, kwa ajili ya watu waliouawa huko El Paso na Dayton, kwa ajili ya familia zenye huzuni, na kwa ajili ya watu wa mitaani ambao wanaistawisha parokia yetu kwa uwepo wa Mungu katikati yetu.

***Sr. Regina Siegfried,ASC***



# Kutangazwa Mtakatifu Kardinali Newman huko Roma



Sherehe ya kutangazwa Mtakatifu John Henry Newman, pamoja na wanawake watakatifu wanne wa Kanisa, sasa imekamilika; lakini uzoefu wa wakati huu maalum unaendelea kwa shukrani mioyoni mwetu sisi ASC tuliojaliwa kushuhudia tukio hilo. Msisimko wetu ulianza katika siku kabla ya adhimisho wakati kikundi cha watalii kutoka Chuo Kikuu cha Newman kilipowasili kwenye Nyumba Kuu. Walikuwa wamechoka kweli kwani walikuwa wakipanda vilima vya




Roma tangu mapema asubuhi, lakini waliimarika vizuri kupitia Misa ya Kiingereza, ikifuatiwa na chakula cha sherehe pamoja na Uongozi Mkuu na Jumuiya ya kimataifa ya nyumba kuu. Tulimaliza muda wetu wa jioni majira ya saa 9:00 usiku kwa wimbo mfupi wa Frere Jacques katika lugha saba zinazozungumzwa ndani ya nyumba hiyo.

Asubuhi ya Jumapili tulitoka kwenda Vatican, lakini tuligundua kwamba njia yetu ya basi ilikuwa imefutwa kwa sababu ya mbio za michezo katika eneo letu, kwa hivyo tukasafiri kwa njia ya treni ya kupita chini ya ardhi, safari ambayo hatukuipanga. Treni hiyo ya kupita chini ya ardhi ilitupeleka hadi kwenye kituo kilicho karibu na Kanisa Kuu la Mt. Petro ambako tuliungana na maelfu ya watu waliokuwa wanaharakisha kwenda kwenye kiwanja cha Mt. Petro. Baada ya kupita kwenye sehemu ya kukaguliwa kwa ajili ya usalama, tulipata viti vilivyokuwa juani na tulifurahia masaa kadhaa ya kushirikishana na watu ambao kama sisi walikuwa pale kushiriki tukio hili. Ili kujiweka sawa, tulisali Rozari kwa sauti kabla ya sherehe kuanza.

Sherehe ya kutangazwa watakatifu ilikuwa si ya kifahari sana. Kardinali Mkuu anayehusika na Kesi za Watakatifu alimwomba Baba Mtakatifu kuwapokea wateule watano kwa ajili ya kutangazwa watakatifu na kuwaandika katika orodha ya Watakatifu. Baada ya kusaliwa Litania ya Watakatifu, Papa Francesco alizungumzia njia rahisi kwa ajili ya kutangazwa watakatifu. Kwaya iliimba Alleluia, na tuliingia moja kwa moja kwenye utukufu na matiririko mzima wa Ibada ya Misa. Kijitabu kilitolewa kwa kila mshiriki ili tuweze kuungana na kwaya ya Gregori katika kuimba. Wakati wa Komunyo, kwaya iliimba wimbo wa Newman "lead, Kindly Light" kwa Kiitaliano.

Mwishoni mwa sherehe, Baba Mtakatifu alipanda kwenye gari yake ya kipapa na akazungukia umati mara mbili, akitabasamu na kutoa baraka zake. Tulimaliza kwa furaha na kupata mang'amuzi makubwa.





**_Sr. Gabrielle Rowe, ASC_**

Eneo la Bara: Ulaya
Region ya Italia

# ASC "kurudi" Morino



Masista Waabuduo Damu ya Kristo walirudi Morino kusherehekea sherehe ya mtakatifu mlinzi wa jiji hilo. Kulikuwa na mapokezi motomoto na yenye hisia toka kwa jamii nzima na kifungo cha upendo bado kiko hai na kushirikishwa kwa kiasi kikubwa na mji wetu kwa Masista Waabuduo Damu Azizi!

Inatosha kukumbuka kuwa nyumba huko Morino (iliyofungwa miaka michache iliyopita kwa sababu ya ukosefu wa watawa katika Shirika) ilianzishwa na Mtakatifu Maria De Mattias katika kipindi hicho cha zamani mnamo Novemba 1841, nyumba ya tatu ya misioni baada ya ile ya Vallecorsa na Pescasseroli.

Kwa mwongo wa zaidi ya miaka 150, uwepo wa Waabuduo ulienea katika sekta mbali mbali: shughuli za parokia, shule, shughuli za kielimu na burudani, kazi za kufuma na kudarizi, huduma kwa wazee, n.k. bila shaka, yote hayo yalikuwa na athari kijamii na kiutamaduni katika mji na katika maisha ya jamii.

Kufungwa kwa nyumba za watawa za Morino na Grancia kulifanya kukosekana kwa vituo muhimu vya kukusanyika kwa watu, kwa namna ya pekee kwa vijana, ingawa fursa zinatafutwa ili kuendeleza mawasiliano na Masista ambao waliwahi kufanya kazi Morino kwa ukarimu usioweza kusahaulika (mfano, sherehe ya maadhimisho ya miaka 150 ya kifo cha Mtakatifu Maria Mattias mnamo Agosti 2016, ziara za mara kwa mara kwenye makaburi ya Acuto, nk.)

Inaonekana kwa asili na uzoefu, huwa kuna kukaribisha uwakilishi wa Waabuduo kushinda siku zima kwa ajili ya sherehe huko Morino, hasa kwa kusudi la kuendeleza mshikamano, na mazungumzo huru ya pamoja yanayoshirikisha idadi kubwa ya watu.

Ziara ilifanyika mnamo Septemba 7 kwenye sikukuu ya mtakatifu wetu msimamizi.

Masista, kutoka katika nyumba za Acuto (Masista Adelfe, Antonietta na Cesida), Sora (Masista Carmina na Silvana, na kutoka Nyumba Kuu huko Roma (Sista Teresina) waliwakilisha vizazi tofauti vya masista ambao walikuwa kwenye nyumba ya Morino kwa muda wa nusu karne!

Kundi la watoto likiongozwa na makatekista wao, akina mama wengi na watu wengine wa mji wetu waliwakaribisha katika ukumbi wa parokia.

Padre Bernardo, mchungaji, pia aliwakaribisha kwa furaha na kwa mlio wa muda wa kengele za kanisa wakati walipokuwa wakiingi Morino.

Mkusanyiko huo ulikuwa katika roho ya sherehe na unyenyekevu wa kifamila. Baada ya salamu za ufunguzi na kumbukumbu fupi ya historia ya taasisi ya watawa wa Damu ya Azizi - iliyoelezwa na Sr. Adelfe, vijana walihusishwa katika nyimbo na michezo mbali mbali.

Wahamasishaji wa kikundi hicho, Masista na hasa Sr. Antonietta Loreti wanajivunia huduma tukuka ya kufundisha kwa muda mrefu katika shule ya awali ya Morino nyakati ambapo shule ya awali iliongozwa na Masista.

Kutembelea huko kulijumuisha pia nyakati za mambo ya kiroho. Masista walishiriki kwenye kilele cha adhimisho la Misa na maandamano kupitia barabara za mji.

Kwa kweli, maadhimisho ya sikukuu ya mtakatifu mlinzi wa mji alisaidia kutoa mwonekano mzuri wa tukio hilo. Kulikuwa na salamu nyingi na hisia zilizojaa kumbukumbu zilizoibuka kutokana na masimulizi ya watu ambao waliowafahamu na walioweza kutembelea nyumba ya Masista miaka yote iliyopita.

Siku hiyo pia uliandaliwa muda wa kuweza kufurahi pamoja karibu na Maporomoko ya Zompo lo Schioppo. Baadhi ya waumini walihudhuria kwa ajili ya kumbukumbu ya kupendeza na kwa ajili ya mbio za kumbukumbu ya miaka iliyopita ya picha, nyuso, matukio ya maisha, n.k.

Ziara ya Masista huko Morino ilimalizika kwa ushiriki katika ibada ya kuondolewa kwa sanamu ya Mtoto Maria na kusali Rozari.

Sr. Adelfe aliwashukuru watu wa mji huo kwa niaba ya wote kwa upendo na umakini kwa Shirika, ambao wanaudhihirisha kupitia ziara zao za mara kwa mara katika jumuiya ya Acuto, kwa kumbukumbu yao kwa Masista wengi, ambao, kwa utaratibu kamili kadiri ya "Kanuni" za Mwanzilishi, walijitoa katika huduma kwa ajili ya jirani yao mpendwa katika jamii ya Morino ambayo imekuwa sehemu ya kumbukumbu kwa eneo hilo. Morino inatajwa katika historia ya Shirika na inafahamika na kupendwa na Masista wengi.

Tukio hili liliratibiwa kwa ufanisi na Profesa Santina Ferrera kwa kushirikiana nami niliyeandika.

***Anna Giovarruscio***

# Miti ya Mizeituni ya Maarifa

Methali ya zamani ya Wamarekani asilia inasema hivi: **"Haturithi ardhi kutoka kwa babu zetu, tunaikopa kutoka kwa watoto wetu. Ni jukumu letu kuwarudishia."**




Ndio, hili ndilo jukumu letu na la vizazi vijavyo.

Kwa wakati huu, tunazidi kusikia juu ya mabadiliko ya hali ya hewa kutokana na uchafuzi wa mazingira. Tukio la "Wiki kwa ajili ya Wakati Ujao" lililoadhimishwa katika nchi mbali mbali siku hizi lilitoa angalisho kwa ulimwengu wote kuhusu uharibifu wote ambao huufanya ulimwengu wetu utaabike kwa sababu ya ufujaji wa rasilimali zake. Inatosha kufikiria juu ya matundu kwenye safu ya ozoni, kuyeyuka kwa barafu na mabadiliko yote ya hali ya hewa yanayosababishwa nayo.

Inafaa kutambu kwamba wanachofanya vijana ni muhimu. Kijana wa Sweden Greta Thunberg alianza harakati za kimataifa ambazo kinatikisa dhamiri ya kila mtu kwa matumaini kwamba watu wote hasa wenye nguvu wa dunia wataanza kutekeleza mikakati ya kulinda sayari.

Taasisi ya Damu Azizi ya Bari, chini ya uongozi makini wa Sista **Giuseppina Fragasso**, kila wakati imekuwa ikiamini katika umuhimu wa kukuza ufafamu wa dhamiri changa za wanafunzi kwa ajili ya kuheshimu mazingira na utunzaji wake. Kwa kweli, katika maneno yake ya ufunguzi wa mwaka wa Masomo, Sista Giuseppina alisisitiza kuwa "watoto hawa watakuwa watu wazima wa kesho ambao watahitaji kufanya maamuzi ili kulinda dunia. Kwa hivyo, elimu yao ni muhimu. "Kuhusu hili, **Taasisi ya Damu Azizi** kamwe haikosi nafasi ya kuhamasisha matukio kwa ajili ya kusudi hili. Kwa kweli, mwishoni mwa kipindi cha kipupwe kilichopita wanafunzi wa mikondo miwili wa darasa la kwanza walipanda miti miwili ya mizeituni kwenye bustani ya shule.

kilikuwa ni kitendo cha kawaida chenye maana mbili, maana ya kwanza ni kujifunza na ya pili ni ya ishara. Katika muktadha wa kujifunza, kama tulivyosema hapo juu, kusudi lilikuwa ni kukuza uelewa wa watoto kuhusu mazingira asilia na kuwafanya wayaheshimu.

Kwa mtazamo wa ishara, itakumbusha safari hii mpya ya maisha ambayo ni shule.

Mti wa mzeituni ulichaguliwa kwa sababu ni mti muhimu sana katika utamaduni wetu wa kidini na kijamii. Miti hiyo iliyochaguliwa ni aina ya "Bambina", asili ya Apulian ya Alta Murgia, ambao mafuta yake yana utajiri mwingi wenye polyphenols, mafuta yanayoyeyuka kwa urahisi na yenye ladha nzuri ambayo, kulingana na desturi, yalitumiwa wakati wa kuwalisha watoto na yalikuwa kwa ajili ya chakula cha watoto.

Hivyo jina "Bambina" (mtoto), ni kutaka kumaanisha kuwa, kuelewa safari ya masomo ni kama kulishwa.

Vibao viwili vya mawe vilivyotengenezwa na mwanasanaa Caterina Giusy Didonna viliwekwa chini ya mizeituni miwili michanga ili kukumbuka tukio hili. Vibao vina majani mengi ya rangi mjuu yake yanayowakilisha idadi ya watoto kutoka mikondo miwili ya darasa la kwanza. Wakati wa miezi hii ya majira ya joto, mizeituni michanga iliimarika na kurefuka na kuwafanya watoto ambao walikuwa wamepanda kufurahi na kushangaa. Dunia ni zawadi kutoka kwa Mungu, lazima tuiheshimu ...

Tuanze kupanda miti na siyo kuikata.

***Giuseppe Quagliara***
*Mzazi wa mwanafunzi shule ya Msingi*



# "Taa tano za Mungu"

### *Aima: damu kutoka Amerika hadi Liberia ya "taa tano za Mungu"*

Weupe wa uso wa Kanisa Kuu la Mt. Nicola na wekundu wa wachezaji vijana walihitimisha siku ya Muungano wa Damu ya Kristo waliojitolea Damu yao wenyewe kutoka sehemu nyingi za kusini mwa Italia (Puglia, Calabria, Basilicata). Vikundi vinavyofuata tasaufi ya Damu ya Kristo viliongozwa na Waabuduo Damu ya Kristo na Wamisionari wa Damu Azizi, katika mwezi wa Oktoba huko Bari, walikuwa na siku ya mkutano, tafakari na sherehe. Karibu watu 300 walishiriki katika "Aima"/"Damu": kipindi cha asubuhi kilichukuliwa na Padre Luigi Maria Epicoco, maarufu kwa mjadala wake kuhusu Injili kwenye mitandao ya kijamii na katika vitabu vingi alivyochapisha vinavyosaidia kuelewa vizuri mada za imani, lilifuatia adhimisho la Misa katika Kanisa Kuu la Mtakatifu Nikola, mtakatifu mlinzi wa Bari, mtakatifu wa umoja wa makanisa ya Kikristo na ukarimu.



Mwishoni mwa Misa, vijana wa parokia ya Damu Azizi, Bari, pamoja na kikundi cha wachezaji wa parokia wakiongozwa na mwalimu Katia Laguaragnella, walihitimisha hafla hii kwa kusoma na kucheza. Wekundu wa nyuzi na nguo za vijana wachezaji kwa utamu zilisindikiza masomo kuhusu Waabuduo watano wa Damu ya Kristo ambao kwa maisha yao kwa hakika walitoa maana halisi ya zawadi. Wekundu ambao waliupeperusha wakati wa kucheza katika nota za wimbo "Duara la maisha" uliochukuliwa kutoka sinema ya Lion King, baadhi ya masoma yalikumbushia maisha ya Sr. Mary Joel, sr. Shirley, S. Kathleen, sr. Agnes na sr. Barbara Ann. Masista Waamerika watano Waabuduo Damu ya Kristo ambao kweli walitoa maisha yao kwa ajili ya mpendwa jirani. Matone matano ya damu ambayo yanamshuhudia Kristo.

Waabuduo hawa watano wanafikiriwa kuwa mashahidi wa imani: walitoa maisha yao huko Liberia katika miaka ya vita ya ndani ya umwagaji damu, wakiwasaidia watoto na wakitoa msaada kwa wanawake wengi. Daima walibaki wakishikilia utume katika ardhi hii ya Afrika na inaweza kusemwa kwamba hawakuogopa mapigano ya vita ambapo walijibu kwa upendo na sala. Uzuri wao uliangamizwa katika shambulio la bunduki mnamo Oktoba 1992 huko Monrovia, mji mkuu wa Liberia.

Wanawakilisha uhai wa watu watano ambao hawakusimama kwa ubaya, hawakukimbia kutoka katika vita hiyo iliyoharibu nchi, bali waliendelea kutibu watu na kuwakaribisha. Kwa hakika wanaweza kufananishwa na taa tano, kama vile zile nyota tano zilizowekwe kwenye ngazi za Kanisa Kuu la Mt. Nicola, nyota tano ambazo daima zitalishwa kwa moto wa Mungu. Ushuhuda wao wa "damu" pamoja na kuleta uhai, kama ilivyotokea wakati wa siku ya "Damu", ni ishara kwa waamini wote kutazama maisha kwa macho ya upendo.

***Sr. Francesca Palamà, ASC***

# Sauti za Amazon Zilisikika Roma

Nyumba yetu inaungua. Mapafu yetu yamejaa moshi. Oksijeni inakatwa mti mmoja hadi mwingine. Maji yetu yanachafuliwa; samaki wanakufa. Maendeleo yanakua yakiacha uharibifu na kifo katika kuinuka kwake. Wale wanaopinga wanakumbana na kukamatwa au kifo. Nani atasikia kilio cha Msitu wa Amazon? Papa Francis anasema tunataka kukisikia, kwa hiyo aliwakusanya pamoja viongozi wa dini wa nchi za bonde la Amazon huko Latin America kuwasikiliza.

Maaskofu wanapokuwa wakikutana katika Sinodi Oktoba 6 - 27, mjini pote sauti zinazungumza katika vikundi vidogo juu ya mada mbali mbali - zote ziko wazi kwa umma. Watu wengi wa Amazoni wamekuja Roma, wengine wakiwa na nyuso zilizopakwa rangi na kofia za manyoya. Sista Rani Padayattil, ASC na Marcia Kruse, ASC walisikia “Sauti ya Amazon” katika Chuo Kikuu cha Antonianum, Oktoba 5. Mabalozi wa Peru na Colombia Vatikani, na balozi wa Peru nchini Italia walitoa tathmini yao ya tatizo kulingana na mtazamo wao. Kisha tukasikia ushuhuda kutoka kwa watu wanaoishi na kufanya kazi moja kwa moja na watu ambao wanaishi katika maeneo ya Amazon: Masista wa Brazil, Ndugu na Kiongozi wa Jumuiya. Maneno yao yaligusa mioyo yetu na kusukuma akili zetu ili kuwa sehemu ya suluhisho la tatizo hili kubwa.

Mzozo mkubwa uko kwenye mitazamo ya ulimwengu. Upande mmoja unaona dunia kama kitu cha kutumika kwa faida. Upande mwingine huona kila kitu kuwa kitakatifu, cha kutumiwa kwa heshima na sio kuharibiwa. Mwingine huona maendeleo, ambapo wengine huona uharibifu. Wakati ulimwengu wa kisasa unaingia, wazazi lazima waamue kupeleka watoto wao shule au kubaki nao nyumbani ili kujifunza tunu za maadili ya ukoo wao. Mzungumzaji mmoja alisimulia hadithi ya mwenyeji ambaye alienda Ulaya na akarudi akisema “Watu maskini! Hawana chochote ila pesa. “Mwingine alisema kuwa Amazon ni mapafu ya ulimwengu, lakini ina saratani: unyonyaji. Sista alisimulia juu ya uhalifu uliopangwa ambao unafanya kazi kwa kuwaepusha na hatia wanaochukua ardhi, na waadhirika wanatuhumiwa kama wahalifu. Polisi wanalinda shughuli za ukataji miti, wanawalinda wanyonyaji. Waandamanaji wanakamatwa. Sehemu kubwa ya misitu imesafishwa kwa ajili ya kilimo, mifugo, ukataji wa magogo na madini, na zaidi msimu huu wa kiangazi kuliko wakati wowote uliopita.

Kwa hiyo tunasali, hasa wakati wa sinodi hii ili kwamba Sauti za Amazon zisikike na kusikilizwa, la sivyo saratani yake itaishia kutuua sisi sote.

***Sr. Marcia Kruse, ASC***









## Kalenda ya Uongozi Mkuu

**Oktoba 30 –** Sr. Nadia Coppa na Sr. Manuela Nocco: watafanya mkutano kwa njia ya Skype na Tume inayotafiti matumizi ya muda mrefu ya Nyumba Kuu

**Novemba 3 - 16 –** Sr. Nadia Coppa na Sr. Dani Brought: watakuwa kwenye Ziara ya kichungaji huko Argentina

**Novemba 18 – Desemba 1-** Sr. Nadia Coppa na Sr. Dani Brought: watashiriki kwenye Mkutano wa Uchaguzi huko Brazil



## Siku za Kuzaliwa: Tusherehekee Maisha

70

**Sr. Judith Kuman** 24/11/1949 Schaan

80

**Sr. Maria Cipriani** 17/11/1939 Italia

## Mikutano ya Region




*Novemba 21 - 25*

Mkutano wa Uchaguzi **Brazil**

## Waliorudi Nyumbani kwa Baba



| | | |
|---|---|---|
| 04/10/2019 | **Sr. Maria Armillotta** | Italia |
| 20/10/2019 | **Sr. Gabriela Kretz** | Schaan |
| 25/10/2019 | **Sr. Anna Maria Amorino** | Italia |
| 26/10/2019 | **Sr. Margherita Cristantielli** | Italia |


**Gazeti la Kimataifa**

*Waabuduo Damu ya Kristo*

..Kwa Neno Lako..

**Habiri ya kila mwezi**

*na*

***Waabuduo Damu ya Kristo***

***Mawasiliano ya Kimataifa - Uongozi Mkuu***

Via Maria De Mattias, 10 - 00183 ROMA

**Mwaka XXI, N. 10, Novemba 2019**

*Kamati ya wahariri*

**Maria Grazia Boccamazzo, ASC**

**Debora Brunetti**

Tafsiri na

***Sr. Klementina Barbić*** *- Kikroeshia*

***Sr. Betty Adams*** *- Kiingereza*

***Sr. Martina Marco*** *- Kiswahili*

***Sr. Bozena Hulisz*** *- Kipolishi*

***Sr. Clara Albuquerque*** *- Kireno*

***Sr. Miriam Ortiz*** *- Kihispania*

***Sr. Johanna Rubin*** *- Kijerumani*